East African Journal of Swahili Studies, Volume 5, Issue 2, 2022
Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1003

East African Journal of Swahili Studies
eajss.eanso.org
Volume 5, Issue 2, 2022
Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# Sayansi katika Tamthiliya ya Kiswahili: Uchunguzi Kifani wa Tamthiliya ya Orodha

*Deogratius Francis Mkawe[1*] & Dkt. Mohamed Omary Maguo, PhD[2]*

[1] Chuo Kikuu cha Kikatoliki Mwenge, S.L.P. 1226, Moshi – Kilimanjaro, Tanzania.
[2] Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, S.L.P. 23409, Dar es Salaam, Tanzania.
[*] ORCID ID https://orcid.org/0000-0002-6848-6241; Barua pepe ya mawasiliano: mkawedeogratius@gmail.com

**DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1003**

**Tarehe ya Uchapishaji:**

*12 Desemba 2022*

**Istilahi Muhimu**:

*Sayansi, Mbinu ya Utatuzi wa Tatizo, Mtindo wa Usayansi, Orodha, Mwingiliano matini, Mtindo wa Uhakiki, Ujaribizi na Taarifu.*

**IKISIRI**

Makala hii inahusu uhakiki wa Sayansi katika Tamthiliya ya Kiswahili, mifano kutoka tamthiliya ya *Orodha*. Ni moja ya makala chache katika mfululizo wa uchambuzi wa masuala ya kisayansi katika Tamthiliya na Fasihi ya Kiswahili kwa ujumla. Lengo la makala hii ya utafiti ni kueleza sifa fumbatwa za kisayansi zitakazopelekea kuundwa kwa mtindo mpya wa uhakiki. Mitindo ya uhalisia, uhistoria, sosiolojia, umuundo, saikolojia, falsafa, uhalisia mazingaombwe kutaja chache, imetumika kwa muda mrefu katika ulimwengu wa uhakiki. Nadharia ya mwingiliano matini imeongoza uchambuzi huu hususani kupitia usemezano wa matini. Maelezo ya ufafanuzi wa masuala ya sayansi kutoka katika taaluma za fizikia, baiolojia na kemia yalitumika kuwaongoza wachambuzi kuweka alama na kudondoa nukuu zilizofumbata sayansi. Data kuhusu masuala ya sayansi kutoka taaluma za sayansi kavu na taarifu ya tamthiliya zilikusanywa kupitia mbinu ya usomaji makini. Matokeo yameonesha kuwa, juhudi za kuisaka orodha au barua iliyoelezwa na mtunzi, mfasiri na wahakiki wa tamthiliya kuwa ya kuchekesha ni ya kisayansi. Wahusika Padri James, Bw. Chaka Ecko, Salimu, Juma na Kitunda wanaisaka orodha kwa kutumia mbinu ya sayansi ya utatuzi wa tatizo. Wahusika hawa wanahaha kutatua tatizo la kuipata orodha iliyoandikwa na Furaha, binti waliyetembea naye kimapenzi. Msako unatokana na hofu yao kubwa ya kutajwa kwa majina kuwa walimuambukiza ugonjwa wa UKIMWI. Mwanasayansi hufanya uchunguzi hatua kwa hatua pindi anapokabiliwa na tatizo ili kulitatua, hivyo Padri James, Bw. Chaka Ecko, Salimu, Bw. Juma na Kitunda ni wanasayansi. Sayansi hii haitajwi wazi na wahusika, mwandishi, mfasiri au wachambuzi tangulizi. Tamthiliya hii pia haikupewa sifa ya kuwa na sayansi, hadhi inayopewa na makala hii. Makala imeuweka katika ujaribizi

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

uchambuzi wa mtindo wa usayansi kupitia mbinu ya sayansi ya utatuzi wa tatizo. Tabia hii jaribizi ya uchambuzi inasaidia wasomaji kuelewa wahusika wanavyotatua matatizo binafsi na, au jamii ambayo kwa kiasi kikubwa ni malengo ya uandishi wa kazi ya fasihi.

**APA CITATION**

Mkawe, D. F. & Maguo, M. O. (2022). Sayansi katika Tamthiliya ya Kiswahili: Uchunguzi Kifani wa Tamthiliya ya Orodha. *East African Journal of Swahili Studies*, *5*(2), 100-109. https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1003.

**CHICAGO CITATION**

Mkawe, Deogratius Francis and Mohamed Omary Maguo. 2022. "Sayansi katika Tamthiliya ya Kiswahili: Uchunguzi Kifani wa Tamthiliya ya Orodha". *East African Journal of Swahili Studies* 5 (2), 100-109. https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1003.

**HARVARD CITATION**

Mkawe, D. F. & Maguo, M. O. (2022) "Sayansi katika Tamthiliya ya Kiswahili: Uchunguzi Kifani wa Tamthiliya ya Orodha", *East African Journal of Swahili Studies*, 5(2), pp. 100-109. doi: 10.37284/jammk.5.2.1003.

**IEEE CITATION**

D. F. Mkawe & M. O. Maguo "Sayansi katika Tamthiliya ya Kiswahili: Uchunguzi Kifani wa Tamthiliya ya Orodha", *EAJSS*, vol. 5, no. 2, pp. 100-109, Dec. 2022.

**MLA CITATION**

Mkawe, Deogratius Francis & Mohamed Omary Maguo. "Sayansi katika Tamthiliya ya Kiswahili: Uchunguzi Kifani wa Tamthiliya ya Orodha". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 5, no. 2, Dec. 2022, pp. 100-109, doi:10.37284/jammk.5.2.1003.

## UTANGULIZI

### Historia Fupi ya Uhakiki wa Tamthilia ya Kiswahili

Uhakiki wa fasihi na tamthiliya ya Kiswahili umedumu kwa miaka mingi sasa. Si rahisi kutamka bayana lini hasa maisha ya uhakiki yalianza kutokana na kujibainisha katika sura kadhaa. Uhakiki wa fasihi umejibainisha kama kitendo, somo, taaluma au kazi. Sura hizi zimeelezwa na Okpewho (1992) na Mulokozi (1996) kuwataja wachache na kwa pamoja wanakubaliana kuwa uhakiki umedumu tangu kuzaliwa kwa fasihi simulizi. Aghalabu uhakiki unaweza kutokea kwa sababu nyingi kati ya hizo ikiwa ni kuielezea kazi ya fasihi kwa namna tofauti, kufafanua suala ambalo halifahamiki/ halieleweki au kufafanua kauli za jumla. Uhakiki unaweza kuwa wa kitaaluma, kisadfa, kiudhibiti, kutaja chache (Wafula na Njogu, 2007). Tamthiliya ya Kiswahili ni moja kati ya tanzu za Fasihi ya Kiswahili inayofundishwa katika shule za sekondari nchini Tanzania. Wanafunzi wa kidato cha tatu hadi cha sita hupaswa kuchambua tamthiliya tatu kwa lengo la kupata elimu ya maisha na kujibu maswali ya mtihani wa taifa. Tamthiliya ya *Orodha* iliidhinishwa rasmi katika mtaala wa kufundishia Kiswahili kama mojawapo ya tamthiliya za kusomwa na wanafunzi wa kidato cha tatu na nne Tanzania mwaka 2007.

### Kwa nini Masuala ya Sayansi?


Lengo la makala hii ni kuichambua tamthiliya ya *Orodha* (2006) kwa namna tofauti kidogo na iliyozoeleka. Maswali na tahakiki zilizoilenga tamthiliya hii na za Kiswahili zimeegema zaidi katika uchambuzi wa uhalisia, umuundo, historia, sosiolojia, saikolojia, falsafa, uhalisia mazingaombwe kutaja chache. Hali hii imepelekea mawazo tuli katika uga wa uhakiki. Uhakiki wa tamthiliya ya Kiswahili umedhihirisha mielekeo kadhaa ya kiuchambuzi kifani na kimaudhui. Mielekeo tofauti tofauti ya uchambuzi imehusu; utamaduni na wakati, ugonjwa wa UKIMWI, rushwa, ukosefu wa elimu, malezi, uadilifu, uwajibikaji, mvutano wa miji na vijiji, athari ya madawa ya kulevya, mmomonyoko wa maadili, mapenzi, athari ya makundi ya vijana, mitindo na matumizi ya lugha, muundo wa matukio, kutaja chache. Chambuzi za masuala kama haya inajidhihirisha katika chambuzi tangulizi kama ya Mhilu, Nyangwine na Kanyuma (2013) ambazo hutumika katika shule za sekondari.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1003

Uchambuzi wa masuala/ sifa za kisayansi haujatiliwa mkazo mkubwa na wachambuzi tangulizi wa kazi za fasihi ya Kiswahili. Athari chanya na hasi za sayansi katika maadili, makuzi ya vijana na afya zimejadiliwa kwa kiasi fulani kama sehemu ya dhamira zinazojitokeza katika tahakiki mbalimbali. Tahakiki ya Mhilu, Nyangwine na Kanyuma (khj) inadokeza masuala ya upimaji wa damu, matibabu na matumizi ya stirio ya kusikiliza muziki. Udokezwaji huu wa sayansi kupitia dhamira haujatoa mwanga wa kutosha kuhusu mtindo wa uhakiki wa masuala ya kisayansi katika tamthiliya ya Kiswahili. Uchambuzi huu unasaidia kuundwa na kutumiwa kwa mtindo mpya wa uhakiki unaojikita katika sifa za kisayansi, mbinu ya utatuzi wa tatizo ikiwa ni sifa mojawapo. Hata hivyo itiliwe maanani kuwa vipengele vya fani na maudhui haviepukiki katika uchambuzi wowote ule. Hii ni kwa sababu fani na maudhui ni viungo vya mwili wa kazi ya fasihi. Makala hii iliwasilishwa katika kongamano la Kiswahili lililoendeshwa na shule za sekondari mkoani Kilimanjaro, ni zao la utafiti unaonamakinika katika kuchambua masuala au sifa za kisayansi zilizofumbatwa na tamthiliya ya *Orodha*.

Makala hii inazingatia uchambuzi wa pembe tatu. Uchambuzi huu unaelekeza kutolea maelezo ya kina kipengele mahususi/ kidogo/ kimoja cha uchambuzi. Uchambuzi wa pembe tatu unaweza kuelezeka kupitia kielelezo kifuatacho:




Kilelezo hiki kinaelekeza kuwa, mhakiki huanza kwa kuwa na wazo pana kisha kulivunja vunja vipande hadi kufikia wazo dogo mahususi. Wazo mahususi ndilo hasa mhakiki hulitolea maelezo ya kina baada ya kuisoma taarifu ya kazi ya fasihi na kuweka ithibati zinazothibitisha mawazo yake. Dhana ya sayansi ni pana na masuala/ sifa za kisayansi ni nyingi, hivyo makala hii imejishughulisha na sifa moja tu ya kisayansi ya mbinu ya utatuzi wa tatizo au utafiti wa kimantiki.

**Muhtasari wa Tamthiliya ya *Orodha***

Tamthiliya ya *Orodha* ni tamthiliya iliyotungwa na Steve Reynolds mwaka 2006 na kufasiriwa na Saifu D. Kiango mwaka huo huo. Mtunzi ameielezea kama tamthiliya katika tapo la tanzia-ramsa. Tamthilia hii imefikisha ujumbe mzito wa majonzi kuhusu gonjwa hatari la UKIMWI wakati huo huo ikizua vicheko wakati wa kutafuta orodha. Katika utangulizi wa taarifu ya tamthiliya, imeelezwa bayana kuwa ni tamthiliya iliyolenga masuala ya Kitanzania na wahusika wa Kitanzania. Vile vile ilielezwa gonjwa la UKIMWI lilikuwa suala muhimu la kutafiti na liliigusa Afrika kwa kiasi kikubwa (Kiango, 2006). Licha ya kuandikwa kwanza kwa lugha ya Kiingereza, *Orodha* imetambuliwa pia kama tamthilia ya Kiswahili (Mhilu, Nyangwine & Kanyuma, khj). Wanaielezea ni tamthilia ya kielimu iliyosawiri mila na desturi za Kiafrika zinavyochangia au kuzuia maambukizi ya ugonjwa huu hatari. Makala imeichukulia kuwa tamthiliya ya Kiswahili licha ya kuwa zao la tafsiri kwa kigezo cha utaifa kwa mujibu wa Madumulla (2009). Anaeleza fasihi ya Kiswahili ni ile inayolenga kumsawiri mtu na maisha yake katika kiwango cha utaifa, na si kiwango finyu cha jamii ndogo. Ni fasihi inayolenga kujenga na kuaridhia mila, desturi, jadi na utamaduni wa mtu katika ngazi ya taifa. Kwa hoja hizo, *Orodha* ni tamthiliya ya Kiswahili inayofikisha kwa Watanzania na Waafrika wote ujumbe mzito wa maambukizi ya ugonjwa wa UKIMWI kwa njia ya kuchekesha. Dhana ya utafiti ilitajwa katika utangulizi kama njia iliyotumiwa na mtunzi na mwandishi kuiumba tamthiliya ya *Orodha* pasipo kuielezea kama imetumiwa na wahusika wake. Mtunzi alikiri kutafiti mazingira ya msichana wa kijijini Tanzania aliyekufa kwa ugonjwa wa UKIMWI kabla ya kuiandika tamthiliya hii. Utangulizi wake hauelezi kama wahusika wake walitumia utafiti kuelezea suala zima la ugonjwa husika.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1003

Juhudi za kuisaka orodha iliyoachwa na Furaha inadhihirisha dai hili hata hivyo ndani yake kumefumbatwa masuala ya kisayansi yasiyopewa hadhi hii na wachambuzi tangulizi. Makala hii fupi, imefuatilia igizo la kuchekesha la kuipata orodha na kufahamu maudhui yake katika kuelekea kutimiza lengo la kueleza sifa za kisayansi zilizofumbatwa. Aidha makala hii inawaachia changamoto wachambuzi wengine kuitumia sifa au sayansi ya mbinu ya utatuzi wa tatizo kufuatilia hatua kwa hatua matatizo yaliyohusu; maambukizi ya ugojwa wa UKIMWI yalivyotokea kwa Furaha, kujibu maswali yaliyowakabili wahusika kuhusu afya ya Furaha, jinsi wazazi walivyokabiliana na badiliko la kitabia la Furaha, jinsi Furaha alivyotimiza kiu ya kuwaelimisha wanakijiji na kudadisi endapo wawili wapendanao walijitunza na wataendeleza mahusiano yao hata baada kutengwa na masuala ya elimu kwa muda mrefu. Vile vile, mbinu ya utatuzi wa tatizo si sayansi pekee inayojitokeza katika tamthiliya ya *Orodha*. Tafiti zaidi zilenge kuchunguza masuala mengine ya kisayansi katika tamthiliya hii na tamthiliya ya Kiswahili kwa ujumla.

## DHANA YA SAYANSI NA NADHARIA ONGOZI

Dhana ya sayansi ni telezi kwa kuwa haina maana moja. Taaluma tofauti tofauti zinaelezea sayansi kwa namna mbalimbali. Sayansi inaelezwa kama mchakato pangilifu wa kutatua tatizo hatua kwa hatua (Singh, 2006; Nichols & Stephens, 2013), matumizi ya namba, fomula na ukokotoaji wa hesabu (Kumar, 2012), isimu/ sayansi ya lugha (Eddington, 2008) na udadisi wa kisaikolojia (Passer & Smith, 2008). Upande wa fasihi, sayansi inatambulika kupita utafiti wa kimantiki, ugunduzi na matumizi ya vifaa vya kisayansi, utabiri wa maendeleo ya vifaa vya kisasa miaka mingi ijayo, utabiri wa vita vya dunia, uelezeaji wa kimantiki wa badiliko la kudumu, matumizi ya wahusika/matukio/njozi za kustaajabisha, safari za mbali kwa muda mfupi sana, kutaja chache (Mulokozi 1996; Roberts, 2002; Mucee, King'ei & Wafula, 2018).

Kwa kuwa dhana hii ni telezi, wahakiki waliongozwa na nadharia ya muingiliano matini ya Julia Kristeva inayoeleza kuwa kila matini ya kifasihi husemezana na matini zilizo na zisizo za kifasihi. Yaani matini ya fasihi imeumbwa kwa kuchota masuala mbalimbali kutoka katika matini nyingine na kuyafinyanga pamoja. Hivyo kuna ufanano fulani unaojitokeza katika kazi za fasihi ulio katika matini nyingine za fasihi na zisizo za fasihi (Haberer, 2007). Mawazo haya ya kinadharia, yamesaidia kusoma kwa makini sayansi inayoelezwa na taaluma zisizo na zilizo za fasihi kuhusu mbinu ya sayansi ya utatuzi wa tatizo na kuyatafuta katika taarifu ya tamthiliya. Kupitia mbinu ya usomaji makini, wachambuzi walisoma masuala ya kisayansi na kubaini yanatawaliwa na mbinu ya utafiti wa kimantiki.

### Sayansi ya Mbinu ya Utatuzi wa Tatizo

Tamthiliya ya *Orodha* inasukumwa mbele na juhudi za kuchekesha za kuisaka orodha iliyoachwa na Furaha. Dhana hii ya msako inadokeza kuwepo na shida inayohitaji ufumbuzi. Wanasayansi wa sayansi kavu; kemia, baiolojia na fizikia wamependekeza mbinu ya utatuzi wa tatizo ambayo ni sifa ya kisayansi. Mbinu hii ya kisayansi ya utatuzi wa tatizo hujumuisha; kutambua tatizo, kuunda nadharia tete/ mabunio, kufanya jaribio, kukusanya data, kuchakata data, kufikia hitimisho na mwisho kabisa inapohitajika kuunda kanuni (Singh, 2006; Eddington, 2008; Kumar 2012; Nichols & Stephens, 2013). Juhudi za kuitafuta orodha zinafanyika kisayansi licha ya kuwa ni za kuchekesha. Hata hivyo si mwandishi, msimulizi au mhusika katika taarifu au wachambuzi tangulizi wanaoipa sifa ya kisayansi au kuona mchakato huo ni wa kisayansi.

Sifa kubwa zimwendee mtunzi na mwandishi kwa ubunifu wake wa hali ya juu wa kutumia muundo rukia katika kuisaka orodha. Muundo huu unafanya jitihada hii kuwa ya mvuto zaidi na kutogundulika kwa wepesi kuwa ni ya kisayansi. Muundo huu unaifanya tamthiliya ya *Orodha* ianzie mwishoni katika msiba kisha kutupeleka katika kiini na baadae mwanzoni mwa mgogoro huu wa kuisaka orodha. Kwa maneno mengine hadithi ilianzia mahali pa kuhitimishia. Juhudi hizi za kuchekesha lakini za kisayansi zinaweza kufuatiliwa na kutolewa maelezo kupitia sifa ya kisayansi ya mbinu ya utatuzi wa tatizo. Msako wa kuchekesha wa orodha iliyoandikwa na kuachwa na Furaha kama wosia kwa jamii umechambuliwa hatua kwa hatua.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1003

Hatua ya kwanza ya sayansi ya mbinu ya utatuzi wa tatizo ni kutambua tatizo. Mhusika wa tamthiliya hupaswa kulitambua tatizo hatua inayopelekea utafiti kufanyika ili kupata ufumbuzi. Barua au orodha iliyoandikwa na Furaha wakati wa mwisho wa uhai wa maisha yake ilizua kizaazaa. Maswali mengi na wasiwasi unabakia kwa wahusika wenzake waliokutana naye kimwili; Bw. Ecko, Padri James, Salim, Bw. Juma na Kitunda. Kwa pamoja wanashindwa kufahamu maudhui ya barua au orodha iliyoachwa wakihofia kuwa wametajwa wazi kwa majina kama watu waliokutana naye kimwili. Zaidi ya hili wanahofia nafasi zao katika jamii kama mwanandoa, mtumishi wa Mungu na mwalimu, wakitambua jamii haitawaelewa walichofanya. Tatizo la kuipata orodha linadhihirika nyakati za mwisho za uhai na baada ya kifo cha Furaha kupitia dondoo zifuatazo;

> *(Watu wote wanamwangalia Padri. Kwenye nyuso zao kuna mchanganyiko wa shauku, kicheko na kuchanganyikiwa. Padre James anauangalia kila uso kwa zamu na, kwa kujua kwamba macho yote yameelekezwa kwake, anarudi nyuma, **usoni mwake akiwa na aina ya tabasamu kavu**)* (uk. 2) *(wachambuzi)*
>
> ***Bw. Ecko:*** *Lazima nikiri nina wasiwasi kuhusu maudhui ya hiyo barua. Mimi nimeoa na ni mfanyabiashara ninayeheshimika. Kwa kweli mimi ni nguzo ya jamii! Hadithi na umbeya havitamsaidia mtu yeyote. Hakika, namkumbuka Furaha kama mwanamke mzuri… Hakuna mwanakijiji atakayelikumbuka hilo!*. (uk. 3)
>
> ***Mwanakijiji wa 1:*** *Furaha ameandika barua ili isomwe wakati atakapokufa!* (uk. 26)
>
> ***Mwanakijiji wa 2:*** *Kwa ajili ya kitu gani?* (uk. 26)
>
> ***Bw. Juma:*** *… (Juma na Ecko wanatazamana kwa namna ya kuwa na hatia)*(uk. 27)
>
> ***Salim:*** *… wanasema kwamba umeandika kitu kama barua hivi… au orodha.* (uk. 28)
>
> ***Salim:*** *Nataka kuiona hiyo barua*. (uk. 30)
>
> ***Bw. Ecko:*** *… Sasa, tuitafute hiyo orodha na kuondoka hapa!* (uk. 33)
>
> ***Padri James:*** *.. bahati mbaya sana! Kusoma barua… orodha… kwa sauti kwenye mazishi! Nani anayejua kinachoweza kutokea kwamba inawezekana… haifai! … Lakini inaweza kuwa wapi?* (uk. 37)
>
> ***Padri James:*** *Sasa, hii orodha inaweza kuwa mahali gani, tena!* (uk. 37)
>
> ***Padri James:*** *… Hizi karatasi ziko wapi? Hizi ni karatasi gani?* (uk. 37)
>
> ***Bw. Ecko:*** *… Hapo si mahali ninapotaka kuwepo, lakini nataka kujua kwenye ile barua mna nini, tena mke wangu pia anakwenda!* (uk. 41)
>
> *(… Salim, akiwa nyuma, anaonekana kuwa na wasiwasi na yuko tayari kujitetea – amelewa kidogo)* (uk. 43)

Data hizi zinaeleza kuwa wahusika walitambua tatizo lililowakabili. Bw. Ecko, Padri James, Salim, Bw. Juma na Kitunda hawakuwa na uhakika barua/ orodha ilibeba ujumbe gani na kama wamenusurika kutajwa wazi kwa majina kama wahusika waliomwambukiza Furaha ugonjwa wa UKIMWI. Hali hii iliwajengea hofu na kwa kutambua nafasi zao katika jamii ilibidi wafanye jitihada kuitafuta na kuipoteza.

Hatua ya pili ya sayansi ya utatuzi wa tatizo ni uundaji nadharia tete au mabunio. Haya ni makisio au mawazo / majibu ya awali ambayo hayajathibitishwa kama yanatatua tatizo. Mabunio kadhaa ya mahali orodha ilipo na nani waliomwambukiza ugonjwa yanajitokeza wakati wa juhudi za kuisaka. Nadharia tete zinajitokeza katika taarifa zifuatazo;

> ***Mwanakijiji wa 1:*** *Wanasema kwamba ni orodha. Inasema kwamba mwanaume alimpa ugojwa huo! Orodha ina kila majina ya kila mwanaume, katika kijiji hiki, ambaye inawezekana alimpa ugonjwa huu! Nimesikia Furaha kamwomba mama yake aisome kwa sauti wakati wa mazishi yake!* (uk. 26)
>
> ***Bw. Ecko:*** *Nadhani, inawezekana kuwamo humu chumbani… kwenye maiti. Vinginevyo, mlango wa pili, sebuleni.* (uk. 32)

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1003

> ***Padri James:*** *Kama si chumbani mwa Furaha… lazima itakuwemo humu! Pengine hapa katika hili kabati!* (uk. 37)

> ***Padre James: …*** *Sasa kama ningeweza kuipata hiyo orodha! Kila kitu kingeokolewa! … Kama si chumbani mwa Furaha… lazima itakuwemo humu! Pengine hapa katika hili kabati!* (uk. 37)

> ***Padri James:*** *… Familia kama hii inaweza hata kuiacha chini ya kochi!* (uk. 37)

> ***Bw. Ecko:*** *… Ulisema nyumba ile ni ndogo, tuna uhakika wa kuipata hiyo orodha.* (uk. 40)

Dondoo hizi zinathibitisha mawazo ya awali waliyokuwanayo Bw. Ecko, Padri James, Salim, Bw. Juma na Kitunda kwamba wametajwa katika barua kwa majina. Kila mmoja alijaribu kufikiri maudhui yake na wapi barua / orodha husika iliyowapa hofu kubwa ingepatikana. Mabunio yanaeleza orodha iliwataja wapenzi wake kwa majina, itapatikana hivyo kujiokoa na ilifichwa chumbani, kabatini na kwenye kochi. Matumizi ya maneno 'Wanasema, nimesikia, nadhani, pengine, kama si, inaweza' yanathibitisha kukosekana kwa hakika ya majibu ya awali.

Majibu ya awali hupaswa kufanyiwa jaribio ili kupata hakika yake. Ni katika hatua hii wahusika Bw. Ecko, Padri James, Salim na Juma wanafanya majaribio mbalimbali ya kutafuta na kuipata orodha. Majaribio yanafanyika kupitia; kuiomba, kuingia na kukagua chumbani, kuuliza swali, kuchunguza kabatini, katika kochi, chungu, katika maiti na hata kuinyakua kwa nguvu.

> ***Padre James:*** *Mama Furaha, ninapinga! Haya ni mazishi na wala si onyesho la pembeni la futuhi! Hapa si mahali pa…* (uk. 3, 43)

> ***Salim:*** *… kama umefanya hivyo… ungenionyesha… au sivyo? … Kwa hiyo, barua ipo! Kwa nini, Furaha? Na kwa nini siwezi kuiona?* (uk. 29)

> *(Giza. Wakati wa usiku. Ukiwacha maiti, chumba ni kitupu. Taratibu, dirisha la chumbani linafunguka. Taratibu na kwa uangalifu Bw. Ecko na Bw. Juma wanaingia. Bw. Juma anaingia mwanzo. Ni dhahiri anatiwa moyo na Ecko. Wanaendesha maongezi yao kwa minong'ono*) (uk. 31)

> ***Bw. Ecko:*** *Wacha kufanya fujo hapa, ingia*. (uk. 31*)*

> ***Bw. Juma:*** *Sawa, tayari niko ndani.* (uk. 31)

> ***Bw. Ecko:*** *… Sikiliza (Kimya) tungaliweza hata kuingia na kundi la tembo au kupiga hodi mlangoni na kusema, tafadhali, bwana tunaiomba orodha ya kihekaya ya Furaha!* (uk. 31)

> ***Bw. Juma:*** *Sidhani kama wamesikia. (Wanasimama kwa uangalifu na kukiangalia chumba kwa makini"* (uk. 31)

> ***Bw. Juma:*** *umeona chochote?* (uk. 32)

> ***Bw. Juma:*** *Angalia kwenye maiti. Mimi nitaangalia makabatini* (uk. 32)

> ***Bw. Ecko:*** *Kwa nini niangalie kwenye maiti? (Anaingalia maiti kwa makini)* (uk 32)

> ***Bw. Juma:*** *Anarudi. Haraka turudi ndani! (Wanashindana kuingia kwenye jeneza)* uk. 33

> ***Bw. Juma:*** *… Tutafute haraka na kuondoka hapa! (Wote wawili wanatoka nje ya jeneza na kutambaa chumbani kote…)* (uk. 34)

> ***Padre James:*** *Na ulisema kwamba Furaha alikuwa… na aina fulani ya ombi la mwisho?*

> ***Padri James:*** *Ningefurahi kuyaona hayo maandishi mapema*. (uk. 36)

> ***Padre James:*** *Hakika, … Na… Naomba uniache peke yangu kwa muda… niyakusanye mawazo yangu… Matakatifu*! (uk. 37)

> ***Padri James:*** *… (Padri James anakwenda haraka kwenye kabati na kuyachunguza madroo harakaharaka) (*uk. 37)

> ***Padre James:*** *… (Mkono wa Padri James ukiwa kwenye madroo, …)* (uk. 37)

> *(Padri James anaanza kukagua kwa hasira kwenye mito ya kochi na viti)* (uk. 38)

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1003

> *(Salim anakimbia mbele na kuipora barua – akishikilia ukurasa mmoja tu – katikati ya mitweto kutoka kwa wanakijiji)* (uk. 43)

Dondoo hizi kutoka katika taarifu / mwili wa tamthiliya, zinathibitisha majaribio ya kisayansi ya kuipata orodha. Kuuliza, kuangalia, kuomba, kupekua sehemu mbalimbali na kunyakua kwa nguvu ni majaribio yaliyofanywa ili kuipata orodha. Matumizi ya neno 'kuyachunguza' kutoka kwa msimulizi anayefahamu kila kitu kuhusu wahusika wake ni ushahidi mwingine wa kutumika kwa sayansi ya mbinu ya utatuzi wa tatizo.

Ukusanyaji wa taarifa hufanyika katika hatua ya nne. Hatua hii imefanyika wakati majaribio ya kuipata orodha yakiendelea. Taarifa mbalimbali zilikusanywa ikiwa ni pamoja na kumwona paka na kuwa na maradhi ya UKIMWI. Taarifa zilikusanywa kwa kutazama kwa macho na kusikiliza kama inavyothibitika katika dondoo hizi;

> ***Mama Furaha:*** *Lakini turudi kwenye suala la msingi. Kabla hajafa, Furaha … aliandika barua hii hapa … na kunipa. Katika barua hii kuna orodha ambayo amesema inadhihirisha yote juu ya mateso na kifo chake… na jinsi alivyokipata kirusi hiki hatari! Alinitaka niisome kwa sauti ili kijiji chote kijifunze kutokana na makosa yake na iwe kama onyo kwa wale watakaotaabika na angamizo hili la kutisha ambalo limeyachukua maisha yake!* (uk. 3, 43)
>
> ***Furaha:*** *Nina UKIMWI, Salim* (uk. 29)
>
> ***Furaha:*** *hapana itabidi, usubiri. (alijibu pindi Salim aliposisitiza kupewa orodha) (uk. 30)*
>
> ***Bw. Juma:*** *Hapana, lakini hapa kuna watu wa kutosha wanaotoa pole. Natumaini wote wamelala! (uk. 31)*
>
> ***Bw. Ecko:*** *Eeeek! Maiti iko kitandani* (uk. 31)
>
> ***Kitunda:*** *… Humu chumbani mna paka!* (uk. 33)
>
> ***Mama Furaha:*** *Furaha aliniomba niseme maneno machache yaliyoandaliwa… Aliacha barua ya kusomwa kwa sauti kwenye ibada.* (uk. 36)
>
> ***Mama Furaha:*** *… Furaha alitaka ionwe na kusikiwa kwa mara ya kwanza kwenye mazishi. Hata sisi hutujaisoma…* (uk. 36)
>
> ***Padri James:*** *Humu hamna kitu!* (uk. 37)
>
> ***Mama Furaha:*** *Mungu ameona inafaa kuhifadhi sehemu ya ujumbe ambao binti yangu amewaachia! (Anaiangalia hiyo barua na tabasamu linaanza kuchanua kwenye midomo yake. Anakohoa na kuanza kusoma kwa sauti). Kwa kijiji changu kipendwa. Nawashukuru kwa kufika kwenu na kuyasikiliza maneno yangu ya mwisho. Msiogope, kwani nadhani maneno haya yanaweza kuwasaidia. Katika ukurasa unaofuata kuna orodha ya vitu ambavyo vilisaidia kuyafupisha maisha yangu, orodha ambayo inaonyesha kwenu nyote ukweli juu ya kifo changu"* (uk. 44)
>
> *Mama (Furaha): Uepukaji …*
>
> *Mwanakijiji wa 2: Kondomu*
>
> ***Bw. Ecko:*** *Uaminifu*
>
> *Mwanakijiji wa 3: Elimu*
>
> ***Padri James:*** *Uwajibikaji*
>
> *Bw. Juma: Ukweli*
>
> ***Salim:*** *Msamaha.* (zote kutoka uk. 44)
>
> ***Salim:*** *Ukosefu wa mambo yote haya ndio ulioniua. Ufuatiliaji wa mambo yote haya unaweza kuwaokoa ninyi na nyote. Chukueni orodha yangu na muinakili. Ipelekeni kwenye vijiji vingine, miji mingine na majiji mengine katika hii nchi yetu nzuri. Wanusuruni watu wetu ili waweze kuyafaidia maisha kikamilifu. Wanusuruni watoto wetu ili wasiwe yatima. Muinusuru Afrika… Afrika yetu nzuri!* (uk. 45)

Taarifa hizi zinaeleza data mbalimbali zilizokusanywa wakati wa jaribio. Data hizi zimeeleza masuala Bw. Ecko, Padri James, Salim, Bw. Juma na Kitunda waliyoyaona au kuyasikia. Wakati wa kusikiliza barua inasomwa data muhimu zilikusanywa zilizoelezea masuala ambayo Furaha hakuyazingatia na kupelekea kifo chake.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1003

Uchakataji wa data hufuata na ulifanyika kwa haraka kutokana na uharaka wa kuipata orodha ili kujinusuru na aibu ambayo ingewapata. Data zilizokusanywa zilifanyiwa uchambuzi kubaini zinaeleza nini kuhusu tatizo la utafiti. Bwa. Ecko, Padri James na Salim walitathimini data kwa vipi zinatatua tatizo la kupata orodha na kufahamu yaliyomo kulingana na taarifa hapa chini;

> ***Bw. Ecko:*** *Amekwishaanza kukauka!* (uk. 32)

> ***Bw. Ecko:*** *Enh! Wacha ntoke hapa. Panakera! (uk. 33)*

> ***Kitunda:*** *Hiyo orodha haisaidii kitu ninapokuwa Dar*! (uk. 33)

> ***Kitunda:*** *Nilijua hili lilikuwa wazo la kipuuzi! (Anaangalia pande zote bila ya matumaini …)* (uk. 33)

> ***Mama:*** *… (Wanakijiji wanatazamana kwa kustaajabu na mkanganyiko)* (uk. 44)

> *(Kimya. Ung'amuzi juu ya ukweli wa ordha unazama katika vichwa vya wanakijiji wakati wakitazamana)* (uk. 44)

Kutoka nje ya chumba katika harakati za kutafuta orodha ni uchakataji wa data unaoonesha walifahamu orodha haipo chumbani. Hivyo ililazimu kutumia namna nyingine ili kuweza kuipata. Vile vile kustaajabu na ukimya kwa wanakijiji ulitokea kutokana na kutotarajia Furaha angeweza kusema ukweli wa mwenendo wake na kuthubutu kuwaelimisha kupitia kifo chake. Uchakataji ulifanyika kwa kufikiri baada ya kubaini orodha ilihusu masuala ya kuepuka ili kujikinga na gonjwa hatari la UKIMWI.

Hitimisho la jitihada hizi za kupata orodha lilitokea pale Salim alipochana ukurasa mmoja wa barua baada ya kuunyakua kutoka mikononi mwa mama Furaha. Bw. Ecko, Padri James, Salim, Bw. Juma na Kitunda walipata hitimisho la kutajwa au kutotajwa kwa majina baada ya kusikia masuala ya kuzingatia kuepuka gonjwa la UKIMWI. Licha ya Salim kuchana ukurasa mmoja, ukurasa uliobakia bado ulibeba ujumbe mzito. Pia vipande vya karatasi vilibaki vikiweza kusomwa na wahusika;

> ***Salim:*** *… (Anauchanachana ukurasa huo na kuvirusha vipande hewani. Hivyo vipande vinaanguka kama theluji). alisema msimulizi* (43)

> *(Kimya cha mshangao. … Wanatoka jukwaani huku kila mhusika akisoma tena neno lake kutoka kwenye ile barua) alisema msimulizi* (uk. 45)

> *Mwanakijiji wa 2: Kondomu.*

> ***Bw. Ecko:*** *Uaminifu.*

> *Mwanakijiji wa 3: Elimu.*

> *Mwanakijiji wa 4: Welewa*

> *Mwanakijiji wa 1: Uwazi*

> ***Kitunda:*** *Uadilifu*

> ***Padri James:*** *Uwajibikaji.*

> *Bw. Juma: Ukweli.*

> ***Mary:*** *Upendo.*

> ***Salim:*** *Msamaha*. (zote kutoka uk. 45)

Hii ni hatua ya mwisho ya kupata ufumbuzi wa tatizo. Hitimisho linapatikana kwa ukurasa mmoja kuchanwa na ukurasa mwingine kusalia wakati mama Furaha akiwasomea wanakijiji orodha. Mwandishi anatumia vyema hali ya hasira ya Salim na kutokuonesha kama Salim alisoma kipande alichofanikiwa kunyakua. Hali hii inatumiwa vyema kwa kuwa mara nyingi katika hasira kufanya maamuzi kwa umakini hakupo. Ingetarajiwa kuwa Salim angesoma ukurusa huo kabla ya kuuchana kufahamu yaliyomo. Hata hivyo juhudi za Salim hazikwamishi lengo la Furaha la kutaka kuwaelimisha wanakijiji. Orodha imeonesha masuala ya kuzingatia kuepuka ugonjwa wa UKIMWI na si majina ya wanaume aliokuwa na mahusiano nao kimapenzi. Wanakijiji pamoja na watafuta orodha wanaishia kusoma yaliyoandikwa katika vipande vilivyochanika. Wakati huu wa kusoma hitimisho linafanyika licha ya kuwa mwandishi hajalielezea kwa uwazi.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1003

## HITIMISHO

Turejelee tena kumpa pongezi mtunzi wa tamthiliya ya *Orodha* kwa kuweza kuificha sayansi ndani ya kichekesho. Utafutaji wa orodha ni wa kuchekesha hali inayosababisha sayansi isionekane kwa wepesi. Sayansi ya mbinu ya kisayansi ya utatuzi wa tatizo imetumiwa na wahusika waliojituhumu kutajwa katika barua kwa kuwa hawakuwa na mwenendo bora na waliojiona si mfano wa kuigwa na jamii yao na jamii halisi. Licha ya kujiona hivyo, tunafunzwa kuwa na maarifa ya kufanya utafiti wa kisayansi kupitia mbinu ya kisayansi ya utatuzi wa tatizo. Hii ni sayansi halisi kutokana na mosi, asili na chimbuko lake ni sayansi kavu, pili inadhihirika machoni pa watumiaji wake na tatu ni ukubalifu iliopata kama sayansi mama. Uchambuzi huu umechangia kueleweka zaidi kwa tamthiliya lengwa kwa kuyapanga matukio katika mtiririko wa moja kwa moja. Uchambuzi unaoongozwa na mtindo wa usayansi wa mbinu ya utatuzi wa tatizo hufanya matukio katika muundo rejeshi kupangika katika muundo wa moja kwa moja/ sahili. Vile vile, umefanikisha kuonesha mtindo mpya wa Usayansi unavyoweza kutumika kutolea maelezo ya kina kuhusu taarifu za fasihi ya Kiswahili. Hata hivyo, mtindo huu hauna budi ujaribiwe zaidi ili wachambuzi wachanga na nguli waweze kuuzoea kuchambua kazi za fasihi ya Kiswahili. Makala imeandikwa kwa ufupi na lugha rahisi ili kuwasaidia wanafunzi wa sekondari kidato cha tatu na nne kuisoma na kuielewa kwa urahisi. Watunzi wa kazi za fasihi ya Kiswahili kupitia Makala hii, watajifunza kutumia mbinu ya sayansi ya utatuzi wa tatizo kutunga kazi mbalimbali za fasihi.

## MAREJEO


Eddington, D. (2008). Linguistic and the Scientific Method. Katika Southwest Journal of Linguistics, Volume 27, number 2. https://www.researchgate.net/publication/228848641_Linguistics_and_the_scientific_method

Haberer, A. (2007). Intertextuality in theory and practice. Katika Journal of Literatura, 49(5), 54-67.https://www.researchgate.net/publication/330572602_Intertextuality_in_Theory_and_Practice

Kiango, S. D. (2006, mfasiri). *Orodha*. Tamthiliya ya Kitanzania. Macmillan Aidan Ltd, Dar es Salaam, Tanzania.

Kumar, V. (2012). Mathematics is Science: A Topic Revisited in Context of FCS of India. Katika Journal of ijmecs, 2012, 6, 17-26. https://www.researchgate.net/publication/272852982

Mhilu, G., Nyangwine, N. na Kanyuma, Y. (2013). *Tahakiki vitabu teule vya fasihi kidato cha 3 na 4: nadharia, uhakiki na maswali*. Nyambari Nyangwine Publisher, Dar-es-Salaam.

Okpewho, I. (1992). African oral literature: Backgrounds, character, and continuity. Bloomington and Indianapolis:Indiana University Press.

Madumulla, J. S. (2009). Riwaya ya kiswahili: Nadharia, historia na misingi ya uchambuzi. Dar es Salaam: Mture Educational Publishers Limited.

Mucee, F. M., King'ei, G. K. na Wafula, K. W. (2018). Mbinu ya Ubunilizi wa Kisayansi katika Riwaya: Bina-Adamu (K. W. Wamitila) NA Babu Alipofufuka (S. A. Mohamed). Katika International Academic Journal of Social Sciences and Education / Speciala Issue 1, pp. 1 – 38. https://www.iajournals.org/articles/iajsse_si1_1_38.pdf

Mulokozi, M. M. (1996). *Utangulizi wa fasihi ya kiswahili.* Chuo Kikuu Huria cha Tanzania: -.

Nichols, A. J. na Stephens, A. H. (2013). The Scientifc Method and the Creative Process: Implications for the K-6 Classroom. Katika Journal for Learning throgh the Arts. 9(1). https://files.eric.ed.gov/fulltext/EJ1018325

Passer, M. W. na Smith, R. E. (2008). Psychology: The study of the mind and behavior. New York: McGraw-Hill Education.

Roberts, A. (2002). *Science fiction: The new critical idiom* (2nd ed.). London and New York: Routlage.


 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1003

Singh, Y. K. (2006). Fundamental of research methodology and statistics. New Delhi, New Age International Publishers

Wafula, R. M. na Njogu, K. (2007). *Nadharia za uhakiki wa fasihi*. Nairobi, the Jomo Kenyata Foundation.-

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.